„Anastasia nilimwona ngomani jana akitembea na kijana fulani kutoka kijiji cha Bukindo. Nafikiri huyo kijana ndiye anaishi naye sasa.“

„Unafhamu anakoishi?“

„Ndiyo. Anaishi karibu na joshu la kukogesha ng'ombe.“

Mulele alirudi nyumbani. Alifhamu sana sehemu hiyo. Alifunga safari kwenda kumtafuta hali akifoka.

„Babu atafufuka kama msichana huyu asiporudi kwangu jua limtege mgongo.“

„Mulele“ Bukelele alipiga kelele.

Alifhamu dua la mzazi lina nguvu.

Jumapili watu walifahamu kwamba Anastasia alitoroshwa huko huko ngomani. Jamaa zake walianza kudharau na kutawanyika wakisema:

„Watu wasiofahamu kulea binti zao matokeo yao haya haya.“

Lakini watu wengi walimtetea Anastasia kwamba alifanya vizuri kutoroka. Tumaini aliposikia habari hii alicheka moyoni, „Nimewatenda!“ Alitosheka. Alifunga safari siku hiyo hiyo kwenda Lutare. Huko, alimsimulia Anastasia jinsi watu wengi walivyomsifu kwamba alifanya vizuri kutoroka. (Uk. 76-77)

*Tumaini wohnt eine Woche lang bei John in Lutare. Er versucht John dazu zu bewegen, mit ihm nach Mwanza zu übersiedeln. „Pesa ninazo“ (S. 81) pflegt er zu John zu sagen. John zögert, weil er im eigenen Haus wohnt und seinen Lebensunterhalt selber finanzieren kann. Doch schließlich gibt er nach.*

*Die Stadt Mwanza gefällt Tumaini und John nicht. Das Nachtleben dort ist fad und die Mädchen auf der Straße sind Schulmädchen. Mit ihnen auch nur zu reden, würde Tumaini und John Ärger einbringen. Anastasia ist dazu besorgt, dass ihre Eltern sie in Mwanza leicht finden könnten.*

*Alle drei entscheiden sich für eine Reise in die Großstadt Dar-es-Salaam, wo sie auch Arbeit finden können. Sie fahren mit einem Bus, wo sie zu Dritt auf einer Bank sitzen. Vor ihnen sitzt eine dicke Frau, die ihrem Kind Pfannkuchen, genannt mandazi, zum Essen gibt, einen nach dem anderen. Kurz danach schreit das Kind. Es möchte aufs Klo. Die Mutter fordert den Busfahrer laut zum Anhalten auf. Beim vierten Mal leisten die anderen Passagiere Widerstand. Dazu kommt ein Missgeschick. An diesem Tag hat es heftig geregnet. Der Bus bleibt im Schlamm stecken. Der Busfahrer bittet die Passagiere auszusteigen und den Bus zu schieben. Alle mit Ausnahme der dicken Frau steigen aus. Die Dicke weigert sich und schreit, dass sie eine Fahrkarte für die Fahrt und nicht für solche Arbeit gekauft habe. Schließlich gelingt es den Passagieren, den Bus wieder in Bewegung zu setzen. Der Bus kommt in Shinyanga an. Tumaini ist erstaunt, Dennis am Busbahnhof zu treffen und vermutet, dass er die Nachricht von Leonilas Schwangerschaft und Anastasias Entführung erhalten habe. Aber Dennis weiß nichts davon.*

„Tumaini!“ Dennis alimpiga kidogo begani.

„Oo! Dennis! Ni wewe!“

„Safari ya kwenda wapi?“

„Dar es Salaam,“ Tumaini alijibu.

„Nimekuja kumpokea mke wangu. Sijui kama umemwona humo ndani ya basi. Mwanamke mnene hivi kidogo.“

„Tumekuja naye“, Anastasia alijibu.

„Anatasia pia yuko humo!“ Dennis alishangaa.

Dennis alipokuwa akisalimiana na Anastasia alimwona mke wake akishuka kutoka basini. Alikwenda kumpokea na kumwelekeza kwenye gari la aina ya Kortina lililokuwa limesimamishwa karibu. Dennis alirudi tena kuzungumza na Tumaini.

Wakati huu Anastasia na Tumaini walikuwa bado wakimshangilia mke wa Dennis. Anastasia alikuwa amekwishamwona. Alimwona wakati alipokuja likizoni na mumewe. Lakini alikuwa amekwishanepa sana. Tumaini hajapata kumwona hata siku moja. Alipokuja likizoni na mumewe, Tumaini alikuwa shuleni. John alikuwa akishangaa peke yake pembeni na alikuwa amesahaulika katika mazungumzo.

„Karibuni wote nyumbani,“ Dennis alisema baada ya kufahamishwa kwa John.

„Tuna safari yetu,“ Tumaini alisema.

„Aisee mimi hapa sipati wageni. Karibu nyumbani, Bwana, hata kwa muda wa nusu saa,“ Dennis alimwomba. (Uk. 86)

*Dennis lebt in einer großen Dienstwohnung, in einem Haus mit Garten. Die Wohnung ist mit Bildern und Plakaten zur Förderung des Ujamaa-Sozialismus geschmückt.*

Kulikuwa na picha nyingi sana ukutani. Picha zenyewe zilikuwa za wakuu wa serikali. Kuanzia Rais hadi mawaziri. Kwa kuwa mawaziri hubadilika mara nyingi picha zilionekana kuwa za zamani. Kulikuwa na makaratasi mengine yaliyokuwa zimetandikwa ukutani. Yalikuwa yameandikwa maneno fulani. Tumaini aliamka kwenda kusoma. Katika karatasi moja yalikuwa maneno haya yameandikwa kwa herufi kubwa.

„Katika nchi yetu, kazi iwe ni jambo la kujivunia. Ulevi, Uvivu na Uzururaji yawe ni mambo ya aibu kwa kila mwananchi.“

„Nyimbo za wanasiasa!“ Tumaini alisema moyoni.

Katika karatasi inengine alisoma maneno yafuatayo:

„Epuka utumiaji mbaya wa fedha zako.“

Chini ya maneno haya kulikuwa kumehorwa picha kama vielelezo. Upande mmoja ulikuwa umeandikwa, „Matumizi mabaya.“ Tumaini alisoma chini ya picha kile: „Anavuna pamba na jamii yake: anapata pesa baada ya kuuza pamba; ananunua baiskeli mbili; anakunywa bia na kutumia pesa yake ovyo; anarudia umaskini kama hapo mwanzo.“ Upande wa „Matumizi bora“ alisoma: „Anavuna pamba na jamii yake; anapata fedha baada ya kuuza pamba; anajenga nyumba ya kisasa; ananunua fanicha na vitanda: anafurahia maisha pamoja na jamii yake.“

„Mm!“, Tumaini aliguna. Alikwenda kukaa. (Uk. 88)

*Sie plaudern ein wenig über Nachrichten von zuhause, doch über Leonilas Schwangerschaft schweigen alle. Dennis erläutert die Ujamaa-Politik. Als er sie fragt: „Hivi ninyi mnafikirije juu ya serikali yetu hii?“ (S. 89) traut sich niemand eine Antwort zu geben, denn sie ahnen, was Dennis beruflich macht. Auf einmal kommt er auf die Chinesen aus der Volksrepublik China zu sprechen: „Wachina wanafanya kazi vizuri sana.“ (S. 89). Anastasia unterbricht das Gespräch mit einer Frage über die Chinesen.*

„Ninasikia kwamba wana macho kama ya paka?“ Anastasia aliuliza.

„Huko pande za Mwanza hawajafika?“ Dennis aliuliza.

„Mimi bado sijawaona,“ alijibu Anastasia. (Uk. 89)

*Dennis wendet sich Tumaini wieder zu.*

Dennis aliona kwamba alikuwa hafaidiki na maswali ya Anastasia. Aligeuza mazungumzo.

„Tumaini, unafanya kazi gani siku hizi?“

„Mimi sifanyi kazi yo yote“.

„Unakwenda Dar es Salaam kutafuta kazi?“

„Hata. Mimi ninatembea tu. Nikiona kwamba hapa Shinyanga maisha ni mazuri ninaweza kuishi humu mjini.“

„Kama ukikata shauri kuishi humu mjini, niambie nikikusaidie kutafuta nyumba ya kupanga. Nyumba ya kupanga siku hizi ni haba sana.“

„Tutaona kesho,“ Tumaini alisema.

„Jambo moja bado sijafahamu,“ Dennis aliuliza, „hivi Anastasia ni mke wako siku hizi?“

„Ndiyo,“ Tumaini alijibu.

Anastasia aliguna kidogo, lakini Tumaini hakisikia. Saa ya kulala ilipofika Tumaini na Anastasia walitayarishwa kitanda kimoja. John alitayarishwa chake katika chumba kingine. (Uk. 89-90).

*Am folgenden Tag erkunden Tumaini und John die Stadt Shinyanga, deren Reichtum auf die Diamanten zurückgeht, die in Mwaui entdeckt wurden.*

Waliona visura wengi. Ingawa mji ulikuwa mdogo Tumaini aliona kwamba ulistahili sifa yake - sifa ya kuwa na visura wengi. Kama kweli walikuwa wakivutwa na almasi ya Mwaui, Tumaini hakuweza kuelewa, isipokuwa aliona kwamba kulikuwa na wasichana wengi wadogo wadogo. Wengi kati yao walikuwa wale waliokomea darasa la saba. Wale wasichana wakimbiliao mijini kwa kuogopa kushika jembe. Ilikuwa saa sita John aliposhtukia amekwisha kumsalimu msichana mmoja shikamoo. Yule msichana aliipokea kwa kurembua macho. Macho yake yalikuwa meupe.

„Mnafanya kazi gani?“ yule msichana aliuliza baada ya kuzungumza nao kwa muda.

„Kwani wafanya kazi ndio wana nini?“ Tumaini alisema.

„Sisi hatufanyi kazi,“ John alijibu.

„Mnaishi wapi?“

„Humu humu mjini, lakini tu wageni kutoka Dar.“

Wakati walipokuwa wakitembea na kuzungumza walijiona wamesimama karibu na bar moja. Tumaini alisoma kibao chake „*Africans' Royal Bar*“.

„Karibu humu ndani tupumzike kidogo,“ Tumaini alimwambia yule msichana.

Yule msichana alitazama saa yake. Aliingia hali akipunguzia upepo kwa kitambaa. Alikuwa akitabasamu. Aliwapitisha barabara hilo makusudi.

„Unakunywa nini?“ Tumaini aliuliza walipokuwa wameingia ndani na kukaa.

„Snow Cap“, alisema yule msichana.

„Na John?“

„Mimi ni Ndovu tu.“

Tumaini alitoa noti ya shilingi mia moja, fimbo ya wanaume. Wanawake wa bar waliokuwa wakifanya humo kazi walimtazama mara mbilimbili kwa tabasamu. Walikunywa mpaka saa nane mchana bar ilipofungwa. Wakati wote ule John alikuwa akijitahidi kumpata huyo msichana. Alifanikiwa. Bar ilipofungwa saa nane waliondoka. John alikuwa amemshika mkono Fatuma - jina la huyo msichana - kuelekea nyumbani kwa Dennis. (Uk. 90-91).

*Dennis und Tumaini sind in eine heftige Auseinandersetzung verwickelt. Dennis kommt auf die turbulenten politischen Konflikte in der Welt zu sprechen, sagt „Dunia uwanja wa fujo“ (S. 92) und fügt hinzu:*

„Sisi wanadamu tu kama majani. Tunaanguka kutoka juu mtini; tunaanguka, tunapepea angani kama unyoya namna hii na kuanguka ... Hakuna atakayerudi juu mtini“. (Uk. 93)

*Für ihn sind Menschen wie Blätter, die vom Baum zu Boden fallen und dort liegenbleiben. Zum Baum können sie nie mehr zurückkehren. Er glaubte früher dass, wenn Menschen ein gutes Leben führen, sie in den Himmel kommen werden. Heute denkt er anders. Die Welt und das Menschenleben bilden ein großes Chaos. Tumaini wirft ihn Pessimismus vor. Für ihn ist das Leben zum Genießen da.*

*Schon in seinen Jugendjahren hatte Dennis wenig Interesse an Beziehungen zu Frauen. In der Schule hatte er nur eine Freundin. Sie hieß Vera. Er sprach sie an und sie zeigte rasch Zuneigung. Sie ist schlank und hübsch und trägt den Spitznamen Rahisi, weil sie leicht zu haben*

*ist. Dennis gegenüber ist sie jedoch sehr zurückhaltend. Mehr als einen Kuss bekommt er von ihr nicht. Auch er ging zu ihr auf Distanz. Nach Beendigung des zwölften Schuljahres gingen sie eigene Wege. Tumaini studiert Politikwissenschaft am Kivukoni College in Dar-es-Salaam, Vera absolviert den Militärdienst bei der Jeshi la Kujenga Taifa (S. 99), macht eine Ausbildung als Sekretärin und bekommt eine Stelle in einem Büro. Seither schickt sie Tumaini Liebesbriefe und Taschengeld.*

*Sie reist nach Dar-es-Salaam, wohnt in einem Hotel und verbringt die Abende mit Tumaini. Zur Arbeitsstelle zurückgekehrt, schreibt sie ihm einen Brief.*

Dennis, kuna wanafunzi wawili wa Chuo Kikuu ambao wamekwisha kunisumbua. Wanataka uchumba nami. Nimewakataa wote kwa ajili yako. Ninakungojea wewe. Ufahamu Dennis, tangu zamani nilijizuia kufanya lolote lile pamoja nawe kwa kuwa nilifahamu kwamba wewe ndiye ulikuwa mchumba wangu wa pekee. Ninafahamu pia kwamba kuna siku itafika ambao ungeweza kunifanyizia lo lote upendalo mimi nikiwa mke wako wa maisha. Siku itafika ambayo usiku utakuwa mfupi na mchana mrefu. Lakini Dennis! Siku niliyokuona huko mjini Dar es Salaam ulikuwa umekwisha badilika. Ulikuwa mzuri sana machoni mwangu. Moyo wangu ulikuwa na njaa yako vile kwamba sikuweza kuvumilia. Nilitoa cho chote nilichokuwa nacho. Labda maji ya bahari ndiyo yamekufanya uwe mweupe vile! Dennis mambo yalitendeka Rex Hotel. Wakati ninapoandika barua hii nimechukua mali yako tumboni mwangu. Ukinitupa sasa, basi, maisha yangu yameharibika. Sina mengi. Pokea picha yangu. V.

Dennis jasho lilimtoka. Alikata shauri kuoa upesi kabla mimba haijawa kubwa. Hakutaka wazazi wake watambue. Mpango wa arusi ulifanywa haraka haraka. Vera alimsaidia Dennis kulipa mahari. (Uk. 99-100)

*Nach der Trauung kehrt Vera an ihren Arbeitsplatz zurück und Dennis ins Kivukoni College. Als er noch dort ist, bringt Vera eine Tochter zur Welt, die auf den Namen Restituta getauft und Resi gerufen wird. Der herkömmlichen Sitte entsprechend wird Vera nunmehr Mama Resi genannt. Dennis bekommt eine hohe Beamtenstellung in Shinyanga. Er, seine Frau und Tochter leben dort gut. Vera vernachlässigt den Haushalt, aber das stört Dennis nicht. Er nimmt dies in Kauf.*

*Tumaini, Anastasia und John fahren nicht nach Dar-es-Salaam, sondern bleiben in Shinyanga. Sie haben zwei Wohnungen angemietet. Tumaini bezahlt die Miete für beide Wohnungen. Eines Tages als Tumaini und John Dennis besuchen wollen, ist Mama Resi allein zu Hause.*

Aliwakaribisha. Kwa kuwa alikuwa mzungumzaji aliweza kuwafanya wakae.

„Tumaini, nina maswali ya kukuuliza,“ Mama Resi alisema.

„Niulize tu,“ Tumaini alijibu.

„Karibu viti basi! Nitakuuliza umesimama?“

Walikaa. Siku hiyo John alikuwa msikilizaji tu.

„Tumaini, nimeskia kwamba umeoa,“ Mama Resi aliuliza, „umemwoa Anastasia. Nimeambiwa na Baba Resi.“

„Ndiyo.“

„Unampenda kweli au labda unamvika kilemba cha ukoka?“

„Anastasia amekwisha kuwa mke wangu. Sina nia kutafuta mwanamke mwingine.“

„Imekwendaje hata ukaoa msichana ambaye hakusoma?“

„Ni mapenzi tu, Mama Resi.“



„Mapenzi gani hayo! Mimi ninafahamu kwa nini umemwoa. Umemwoa ili uweze kumwonea. Unataka mwanamke ambaye unaweza kumwamrisha kama mtoto mdogomdogo, karibu kama mtumwa.“

„Kwa nini unasema hivyo?“

„Ninasema vile kwa sababu ninaamini katika usawa kati ya bwana na mke. Watu waliosoma wanapenda kuoja wasichana ambao hawana elimu ya juu kwa sababu hii. Wale wenye elimu wataolewa na nani?“

„Wewe na Dennis mko sawa?“

„Mimi na bwana wangu tunaamini katika jambo hili la usawa. Hata mimi ninaweza kutoa maoni yangu mbele ya bwana wangu. Dennis anafahamu sana kupika. Tunapeana zamu. Mara nyingi tunabishana mezani. Unacheka! Si jambo la ajabu. Katika jamii ya kizungu utakuta mara nyingi mwanamke ndiye ana sauti zaidi kuliko bwana.“

„Mama Resi, jambo la usawa linakuharibu mawazo yako bure. Jambo la maana katika jamii yo yote ni heshima. Bwana na mke, hata kama wakijidai kwamba wao ni sawa, wasipopeana heshima jamii yao haitakuwa thabiti kamwe.“

„Wewe bado una mawazo ya kizee. Mawazo ya zamani! Zamani mama zetu waionewa. Walipigwa mara nyingi na bwana zao. Jambo kama hili halifai tena katika ulimwengu wetu wa sasa.“

„Mimi ninakubaliana nawe kwamba kuna mambo mengine ambayo yanafaa kuachwa. Lakini kuna mambo mengine yafaayo kutunzwa. Wewe unaelewa usawa labda kwa maana ya kizungu – maana ya kumamrisha, kubishana na kujadiliana. Ubishi ndio mwanzo wa matata. Usawa wa kiafrika ni usawa wa kuheshimiana. Tangu zamani wazazi wetu waliheshimiana. Hii ni dhahiri kabisa. Ndiyo maana walikaa pamoja.“

Wakati huu wote wa mazungumzo Mama Resi alikuwa akizungumza hali akimtazama John. Jambo hili lilikuwa limekwisha muudhi John. Mama Resi alimkonyezea jicho. Aliamka kwenda chumbani mwake. (Uk. 103-105)

*Mama Resi bittet John ihr zu helfen, einen Koffer unter ihrem Bett herauszuholen. Tumaini bleibt im Wohnzimmer. Bald kommt John darauf, was Mama Resi eigentlich will. Sie sperrt die Türe ab. John alipofunguliwa mlango alikuwa kama samaki aliyenusurika. (S. 106).*

*Tumaini ist nicht erwerbstätig, da er geerbtes Geld noch zur Verfügung hat. Bei den Frauen in den Unterhaltungslökalen ist er ein gern gesehener Gast. John nimmt Fatuma zu sich als Mitbewohnerin. Auch sie finanziert Tumaini.*

*Tumaini und John besuchen Dennis. Ihr Gespräch kreist um die Fragen Maendeleo d.h. Fortschritt, Uhuru wa Wanawake, d.h. Frauenrechte und Sheria za Urithi, d.h. Erbrechte. Tumaini äußert seine Ansichten:*

Utamaduni wetu ni tofauti na yule wa kizungu. Jambo la uhuru wa wanawake au usawa kati ya mume na mke linafaa sana watu kama hao. Ukichunguza vizuri lugha nyingi za ulaya utaona kwamba katika lugha zao mwanamke pia anaoa. Utamkuta mwanamke akisema kwamba amemwoa mvulana fulani. Kwa hiyo mambo haya yalikuwa ndani ya utamaduni wao tangu zamani. Ukichunguza lugha za kiafrika utaona kwamba katika lugha nyingi mwanamke kila mara anaolewa tu. Mwanamke hawezi kusema kwamba ameo. Lugha hizi zaonyesha kwamba mwanamke ni mtu wa kutendwa tu. Lakini hali hii itaendelea mpaka lini? Hilo ndilo swali.

„Wewe unafikiri nini juu ya urithi?“ Tumaini aliuliza. „Urithi wa Kiafrika haufai,“ Mama Resi

alidakia. „Mtu akifa jamaa za marehemu wanachukua mali yote na kuwaacha watoto bila kitu cho chote.“ (Uk. 115-116)

*Tumaini unterbricht die Auseinandersetzung und kommt auf den eigentlichen Zweck seines Besuchs zu sprechen.*

„Dennis,“ Tumaini alianza, „nilikuwa na shida kidogo nawe.“

„Shida gani?“ Dennis aliuliza.

„Unaweza kunisindikiza kidogo,“ Tumaini alisema hali akiamka.

Dennis aliamka kumsindikiza.

„Kwa heri na kuonana, Mama Resi,“ Tumaini alimuaga. Mama Resi hakujibu. Yeye pia alitaka kujua siri iliyo ikienda kuzungumzwa nje.

Walipokuwa wamefika mbali kidogo, Tumaini alianza kusema shida yake.

„Siku hizi niko katika hali mbaya sana. Nimejaribu kutafuta kazi lakini sikufanikiwa. Nimekuja kuomba msaada wako, maana ninyi mlioko huko juu mna nguvu zaidi.“

„Kazi!“ Dennis alisema hali ameweka mkono wake juu ya shavu, alijifanya kufikri.

„Ndiyo, kazi,“ Tumaini alisema, „isipokuwa isiwe kazi ya kufagia barabarani“.

Ebe tuone...ee kazi. Ulikuwa wapi zamani. Ofisini mwangu kulikuwa na nafasi tano. Lakini sasa eee...ebu tuone. Nafikiri nimekwisha zigawa zote. Sina uhakika. Hata hivyo nitajaribu. Lakini lazima nimwulize mke wangu kwanza. Huenda yeye akawa anataka nimpe mtu mwingine kazi hiyo. Lakini nitajaribu.“

Dennis alipomwambia mke wake, mke wake alifurahi sana. Aliona kwamba Tumaini alikuwa sasa chini ya mumewe. Hata kama angeita (angejiita?) „Mwenyewe“ mara ishirini, Mama Resi hakujali: alikuwa chini ya mumewe.

„Nilikuwa nakwambia kwamba mtu wako pesa karibu zitamwishia,“ Mama Resi alisema, „sasa umeonaje? Badala yetu sisi kumwambia tumpe kazi amejileta mwenyewe.“

„Ulikuwa ukisema kweli.“

„Inafaa umpe kazi ya kupeleleza watu wapingao serikali katika mabar,“ Mama Resi alitoa wazo. (Uk. 117-118)

*Fatuma erkennt langsam, dass das Geld im Haus knapp wird und macht sich davon. Sie nimmt Kleider von Tumaini und John und auch deren Geld mit. Eines Tages, als sich Tumaini und John auf dem Markt befinden, sehen sie ihre Kleider dort zum Verkauf angeboten. Einige Tage später lernt Tumaini Hadija, eine Mswahili aus Dar-es-Salaam, in der Africans' Royal Bar kennen. Sie ist eine Frau mit Vergangenheit. Von sich selbst pflegte sie zu sagen: „Mwanamume ye yote akilala nami lazima atarudi tena kesho yake“ (S. 121). Eines abends besucht sie Tumaini zu Hause.*

„Tumaini, nimesikia kwamba siku hizi unafanya kazi?“ Hadija aliuliza.

„Kazi gani?“ Tumaini alijifanya kuuliza.

„Mimi nimesikia tu; sijui kazi gani. Nimekuja kukuomba pesa kidogo kama umekwisha pokea. Ninahitaji pesa kwa haraka sana. Mwenye nyumba anadai kodi ya kile chumba.“

„Huwa unalipa kiasi gani?“ Tumaini aliuliza.

„Shilingi hamsini tu.“

„Mwenye nyumba anazihitaji lini?“

„Amenipa siku mbili tu. Hakika usiponipa pesa mimi nitakuja tubanane humu chumbani. Sina vitu vingi sana. Nina kitanda na masanduku mawili tu.“

Jinsi Anastasia alivyotoka jikoni hakuna aliyefahamu, wala hapakuwa na mtu aliyemsikia

akitembea. Walishtukia ukuni ukilia juu ya kichwa cha Hadija.

„Malaya wewe! Toka! Hapa! Wewe ndiye unatuambukiza magonjwa!“

Hadija alienea damu. Alijaribu kusimama ili apambane na Anastasia. Lakini Anastasia aliendelea kumpiga tena na tena kama mtu apigae nyoka. Hadija alianguka chini. John na Tumaini walipokumbuka kumshika Anastasia, Hadija alikuwa amekwisha haribika sura.

„Acha nimwue! Mshenzi! Hii ni dharau kubwa sana! Malaya hawezi kuja kuzungumza mambo yake na bwana wangu mbele yangu! Wazi wazi namna hii! Ala!“ (Uk. 122)

*Es geschieht etwas, das niemand im geringsten erwartet hätte. Hadija hebt ihr Kleid hoch, zieht eine Pistole hervor und schießt auf Anastasia, die bewusstlos zu Boden fällt, und beschimpft sie.*

„Mtoto wa mbwa! Unafikiri bwana wako ana nini! Anakupa nini ambacho mimi sipati! Hufahamu kwamba pesa za bwana wako huwa tunazigawanya!“ (Uk. 122)

*Von Tumaini verlangt sie die Schlüssel zum Koffer, nimmt eintausend Tasania-Schilling mit, schießt alle drei in die Beine und geht weg. Tumaini und John schreien laut um Hilfe. Die Nachbarn kommen und bringen alle drei ins Spital. Dort erfahren sie, dass Hadija in Richtung Tabora abgereist sei.*

*Dennis ist in sein Heimatdorf gereist, um das Haus zu besichtigen, das er bauen ließ. Dort erfährt er, dass Leonila einen Sohn geboren hat und dass Aurelia verlobt ist. Zur gleichen Zeit erhält John eine Einladung von Mama Resi zu Tee und Kuchen. Mit Fatuma und Hadija hat er bereits unglückliche Erfahrungen gemacht. Da er zu Dennis gute Beziehungen pflegt, möchte er mit Mama Resi keine weitere intimen Beziehungen eingehen. Er denkt daran in sein Heimatdorf zurückzukehren, zu heiraten und mit seiner Familie dort zu arbeiten. Er nimmt aber die Einladung an, mit der Absicht dies Mama Resi zu sagen, erliegt aber ihren Reizen und übernachtet bei ihr.*

*Tumaini bekommt eine Arbeit bei der Staatssicherheit. Seine Aufgabe ist es, Gespräche zu belauschen und Äußerungen gegen die nationale Ideologie und die Regierung dem Beamten Dennis zu melden. Er ist somit vielen Gefahren ausgesetzt. Seine Freunde meiden ihn. Überall wohin er geht, zeigt man auf ihn und sagt: „Unamwona huyo Security mkubwa“ (S. 131). Er wird einsam. Er erkennt, dass er sich vom Volk entfremdet. Anastasia und John versuchen ihn zu überzeugen, diese Arbeit aufzugeben und eine andere zu suchen. Er lehnt ihren Vorschlag jedoch ab. Er verdient gut und die Arbeit ist nicht anstrengend. In Shinyanga lebt ein Mann namens Makorobo, der in der ganzen Stadt gefürchtet ist. Er ist bereit, gegen Bezahlung jedes Verbrechen zu begehen, auch Mord. Dem Besitzer der Africans' Royal Bar kommen seine Dienstleistungen jedoch sehr gelegen. Er arrangiert ihn für eine Besprechung. Eines Abends sitzt Tumaini in der Bar und beobachtet die Gäste. Inzwischen führen der Barbesitzer und Makorobo ein vertrauliches Gespräch.*

„Nimekwisha mfahamu,“ Makorobo alisema.

„Sasa kiasi gani?“

„Kwa kuwa mtu huyo nina kisasi naye, unaweza kunipa shilingi elfu moja tu.“

„Elfu moja nyingi sana!“

Wewe hufahamu kwamba ni damu ya mtu?“

„Hapana, mimi sitaki damu yake wala maisha yake. Ninataka umfunze tu, au umfanye ahame.“

„Unataka nini, mkono? Ha! Ha!“

„Zaidi ya mkono!“

„Haya mia saba!“

„Hizi ninaweza kukupa. Lakini jambo hili litendeke upesi.“

„Mimi ninafahamu jinsi ya kuwatengeneza. Nitamtengeneza kesho. Lakini inafaa unipe za kuanzia kama mia mbili hivi.“

„Lete Ndovu moja,“ mwenye bar alimwambia mwanamke pale mbele. Bwana Makoroboi alikunywa pombe yake kwa pupa. Alipomaliza kwa mpigo mmoja bila bilauri aliongozana na mwenye bar nje. Huko nje alimpa Makoroboi shilingi mia mbili. (Uk. 133)

*Am folgenden Tag besucht Mama Resi die Africans' Royal Bar. Dort spricht sie vertraulich mit dem Barbesitzer. Am Abend sitzt Tumaini wieder an seinem gewohnten Platz.*

Saa nne (usiku) aliingia mwanamke mmoja aliyekuwa amevaa vizuri sana, viatu vyenye visigino virefu, na mfuko wa mkononi ulikuwa ukinig'inia chini ya mkono wake wenye saa. Yule mwanamke alipoingia ndani ya bar alitembea kwa mwendo wa kinyonga na kwenda kukaa nyuma kabisa karibu na Tumaini.

„Shikamoo,“ yule mwanamke alisalimu Tumaini.

„Marahaba,“ Tumaini alipokea kwa mashaka.

Yule mwanamke mgeni alimtazama Tumaini kwa macho meupe na tabasamu kidogo. Aliweka mfuko wake juu ya kiti. Alitoa sigara na kuvuta. Wakati huo huo mwanamke wa bar alikuwa amekwisha simama pale mezani.

„Namna gani?“

„Kilimanjaro moja, baridi sana,“ mwanamke mgeni alijibu.

Kilimanjaro iletwa. Wote wawili walikunywa pombe hali wamenyamaza. Mwishowe Tumaini alijiona mjinga. Ulikuwa ujinga kukaa karibu na mwanamke bila kusema neno lo lote.

„Samahani, nafikiri kwamba nimekwisha kukuona mahali fulani,“ Tumaini alianza.

„Unasemaje?“

„Nakumbuka kwamba nimekwisha kukuona mahali fulani,“ alirudia.

„Nini!“

Tumaini alisogea karibu. Alihama na chupa yake.

„Jina lako nani?“ Tumaini aliuliza.

„Mbona unasema kwamba umekwisha kuniona! Uliniona wapi?“

„Kama si Mwanza basi Tabora.“

„Inawezekana maana Mwanza nilikaa muda wa miaka miwili. Nimewahi kuishi Tabora kwa muda wa mwaka mmoja.“

„Lakini dada ni muda mrefu umepita. Nimekwisha sahau jina lako.“

„Jina langu Kristina.“

„Kristina!“

„Ndiyo.“

„Jina zuri sana.“

„Na wewe unaitwaje?“

„Mimi Tumaini Mwenyewe.“

„Ohoo“ Kumbe ndiyo wewe! Nimekwisha sikia jina lako mara nyingi sana humu mjini. Kumbe ndiyo wewe Mwenyewe!“

„Unafahamu jina hili nilipataje?“

„Hata!“

„Zamani nilikuwa nikiiitwa Jingojango.“

Kristina alicheka. Tumaini pia alifahamu kwamba mwanamke akicheka ni hatua moja mbele.

Aliendelea.

„Jina la Mwenyewe nilipata shauri ya pesa; wakati huo nilikuwa na pesa.“ Tumaini alinyamaza kidogo. Aliona kwamba maneno aliyomaliza kusema yalikuwa hayamfai mwanamke. Alijirekebisha.

„Siku hizi sina pesa nyingi. Lakini ninazo za kutosha kuweza kunywa na watu kama nyinyi .“

„Hata sasa inaonekana wazi kwamba una pesa.“

„Kwa hiyo fahamu tu kwamba tutakunywa.“

„Sisi utatuweza?“

„Nimekwisha waweza wanawake wengi sana.“

„Basi tuone mwisho wake!“ Yule mwanamke alijibu.

Tumaini alipotazama chupa chake aliona kwamba pombe ilikuwa imebaki kidogo. Alipotazama ile ya Kristina aliona nayo imekaribia mwisho. Alimwita mwanamke mmoja wa bar kwa mkono.

„Lete Ndovu mbili!“

„Hapana mimi huwa natumia Kilimanjaro tu. Nikichanganya, kichwa kinaniwanga kesho asubuhi.“ „Ndovu moja na Kilimanjaro moja,“ Tumaini alisema.

Yule mwanamke alizileta. Kristina alionekana kuwa mnywaji sana. Tumaini alikuwa amekwisha kunywa bilauri mbili tu ndani ya chupa yake; Kristina aliagiza chupa mbili zaidi.

„Kwa nini unaninunulia mimi pombe?“ Tumaini alisema.

„Mimi huwa nafanya vile. Sitaki kuwanyonya wanaume niwapendao.“ (Uk. 134-136)

*Während sie miteinander sprechen, tritt ein Mann ein, den Tumaini nicht kennt und gibt dem Barbesitzer Geld. Es spendiert zwei Flaschen Bier für Tumaini und die fremde Frau Kristina. Es ist spät. „Zwölf Uhr Mitternacht“, sagt Kristina. Zum ersten Mal sieht Tumaini Kristinas Armbanduhr. Sie ist jener Uhr ähnlich, die er an der Hand von Mama Resi sah. Auch die Handtasche, die Kristina bei sich hat, ist ähnlich jener, die er in der Wohnung von Dennis gesehen hatte. Sie bestellen ein Taxi nach Maganzo. Tumaini hat zwar diesen Ortsnamen irgendwann gehört, kann mit ihm aber nichts anfangen. Sie treffen dort ein.*

„Karibu, nyumba ndiyo hii.“

„Nyumba hii yote ni yako?“

Tumaini alipoingia chumba cha kulala alishangaa kuona kwamba Kristina alikuwa na vitu vingi kama vile.

„Hapana! Siwezi kulala humu!“ Tumaini alisema.

„Kwa nini?“

„Nimesema siwezi!“

„Ebu rudi ndani!“

„Mimi nimesema siwezi!“

Tumaini alikuwa amekwisha ona suruali moja imetundikwa ukutani.

„Suruali hiyo ni ya nani?“

„Ni ya bwana wangu,“ Kristina alisema.

„Unataka mimi nife bure!“

„Unafikiri mimi ni mjinga kuleta bwana mwingine na hali bwana wangu yuko nyumbani.“

„Inawezekana! Bwana wako yuko wapi?“

„Bwana amekwenda Zambia. Atarudi huenda baada ya mwezi mmoja.“

Tumaini alikaa, lakini moyo wake ulikuwa na hofu kubwa kila wakati. Alipokuwa akisikia kitu fulani kama panya, aliamka mara moja kwa woga.

„Sijaona mwanmume mwoga kama wewe!“ Kristina alisema.

Tumaini alilala kitandani. Kristina alizima taa. Ilikuwa karibu kama saa tisa. Tumaini alikuwa

amekwisha tosheka. Alikuwa sasa amelala hali mkono mmoja ametupa juu ya Kristina aliposikia watu wabisha hodi. Tumaini aliamka upesi.

„Nani hao!“ alisema.

„Nyamaza kidogo!“ Kristina alisema.

Alikwenda kuchungulia kwenye tundu la ufunguo.

„Kumbe ni rafiki zangu. Usiwe na mashaka yo yote.“ Kristina aliwasha taa. Alikwenda kufungua mlango. Mara moja watu wanne waliingia ndani ya nyumba na visu mikononi. (Uk. 138-139)

*Tumaini zittert. Der Anführer dieser vier Männer, der eine schäbige Mütze trägt, gibt seinen Leuten Befehl, die Türe zu schließen. Kristina zieht sich an und verlässt das Haus. Sie hat ihren Auftrag ausgeführt. Makorobo fragt Tumaini, ob er sich noch daran erinnert, wie er ihn mit einem Stock geschlagen hat. Er zeigt ihm die Narbe. Tumaini gesteht. Makorobo fordert von seinem Begleiter ein Messer. Tumaini weint und schreit. Makorobo lacht laut. Er fordert Tumaini auf, die Bevölkerung in Shinyanga nicht mehr zu bespitzeln. Das sind die letzten Worte, die Tumaini noch bei vollen Bewusstsein zu hören bekommt. Er wird in der Nähe eines Spitals ausgesetzt. Fröhlich kommt er zu Bewusstsein und beginnt zu schreien. Ein Nachtwächter bringt ihn ins Spital. Mama Resi ist die erste Person, die Anastasia diesbezüglich informiert. Anastasia und John besuchen ihn. Anastasia bringt ihm die freudige Nachricht, dass sie schwanger ist. Tumaini glaubt zwar nicht an eine Heilung, wünscht sich aber, dass das Kind Matata heißen soll. Tumaini erholt sich schließlich doch und kehrt zu Anastasia zurück. Bei einer Besprechung mit Makorobo, Kristina und dem Barbesitzer gibt Mama Resi ihre Enttäuschung kund. Sie steckt Makorobo Geld zu und verlangt Tumainis Tod. Doch Makorobo weigert sich. Er verlässt Shinyanga. Tumaini beginnt ein neues Leben. Er besucht Dennis.*

„Bwana Dennis nimekuja kukushukuru,“ Tumaini alisema.

„Kunishukuru kwa jambo gani?“ Dennis aliuliza.

„Kwa kunipa kazi ambayo mpaka sasa ilikuwa ikiniwezesha kuishi hapa Shinyanga.“

„Kwani hutaki tena kuendelea na kazi?“ Dennis aliuliza kwa mshangao.

„Kazi nitaendelea kufanya. Lakini naomba uniruhusu nijuzuru (*auch* -uzulu) kazi niliyokuwa nikifanya.“

„Kwa nini!“ Mama Resi aliuliza.

„Kuanzia juma lijalo, nitakuwa nikifanya kazi ingine (*auch* nyingine),“ Tumaini alisema.

„Kazi gani?“ Dennis aliuliza.

„Huu ni mwezi wa kumi na moja, Bwana Dennis. Ni mwezi mzuri wa kulima pamba.“ Tumaini alisema.

Mama Resi aliyekuwa anaogopa kwamba labda Tumaini kapata kazi ya juu kuliko ya bwana wake sasa alicheka kidogo.

„Unataka kuwa mkulima. Utawezaje kuishi karibu na mji?“ Dennis aliuliza.

„Nitaishi tu. Ninaweza kuhama baadaye. Ninataka kuwa mtoto wa jua. Nataka jua lichome kwa nguvu za joto kali hii ngozi nyororo ambayo haikuzoea kuhimili tabu ya ulimwengu.“

„Kwa nini umeacha kazi uliyokuwa ukifanya?“ Mama Resi aliuliza. „Ulikuwa ukifanya kazi vizuri sana, na Baba Resi alikuwa akifikiria kukupandisha cheo.“

„Kazi ni nzuri,“ Tumaini alisema, „lakini mimi sasa nataka kufanya kazi nipendayo. Kama ni jambo la kupandishwa cheo, nimekwishajipandisha mwenyewe.“

„Na John utampeleka wapi?“ Mama Resi aliuliza.

„Tutakuwa tukifanya naye kazi pamoja.“

„Ukulima ni kazi yenye tabu sana,“ Mama Resi alisema.

„Ninajua,“ Tumaini alidaka, „na ndiyo maana ninaipenda!“

„Ahsante sana kwa kunijulisha,“ Dennis alisema. „Tutajaribu kutafuta mtu mwingine kuziba pengo hilo.“ (Uk. 149-150)

*Dennis hat es eilig ins Büro. Tumaini und John verabschieden sich, Mama Resi bleibt allein in der Wohnung zurück. Tumaini nimmt ein Darlehen von einer Bank und investiert es in einen Traktor und in ein Grundstück. Anastasia, John und Tumaini arbeiten dort gemeinsam jeden Tag. Eines Tages, als er allein bei der Arbeit war und zum Mittagessen kommt, trifft er Anastasia und John beim Liebesakt an. Am folgenden Tag gibt Tumaini John einen Geldbetrag und verabschiedet sich von ihm. John reist mit dem Bus in Richtung Mwanza.*

*Mama Resi vermisst John. Sie sinnt auf Rache. Eines Tages besucht sie Tumaini. Anastasia und er heißen sie willkommen. Sie bittet Anastasia um ein Glas Wasser. Während Anastasia in der Küche ist, greift sie Tumaini mit einem Küchenmesser an. Er wehrt sich jedoch. Sie kehrt weinend heim, wirft Tumaini einen Versuch vor sie zu vergewaltigen vor und zeigt Dennis ihre Unterwäsche, die Tumaini zerrissen haben soll. Dennis fährt sofort zu Tumaini. Dort erfährt er die Wahrheit und vom Liebesverhältnis zwischen John und Mama Resi. Von der Beziehung zwischen Makoroboi und seiner Ehefrau ist Dennis ohnehin informiert. Eines Tages teilt er seiner Ehefrau mit, dass ihre Mutter krank sei, gibt ihr Geld für die Reise und bringt sie zur Busstation. Das Kind bleibt bei ihm. Er schreibt einen Brief an seinen Schwiegervater und teilt ihn mit, dass er die Ehe mit seiner Tochter Vera beendet habe. Er gibt seiner Tochter einen neuen Namen, nämlich Nyanjala. Er schickt Vera ihren Koffer. Anastasia übernimmt die Fürsorge für das Kind, bis Dennis wieder heiratet. Einige Monate später erhält er von Vera einen Brief, worin sie ihn um eine standesamtliche Scheidung bittet. Dem leistet er Folge. Er heiratet eine junge Frau namens Bernadeta, die früher in seinem Büro arbeitete und ein außereheliches Kind mitbringt. Anastasia bringt eine Tochter zur Welt, die Tabu genannt wird. Die Baumwollfelder von Tumaini bringen eine reiche Ernte hervor. Die Eltern von Dennis und Anastasia kommen zu Besuch und bleiben einige Tage.*

*Zwei Jahre sind vergangen. Tumaini ist als Besitzer einer Baumwoll-Plantage gut etabliert. Er hat zwanzig Arbeiter angestellt und somit freie Zeit für seine Frau und Tochter. Die Arbeiter bekommen die vorgeschriebene Bezahlung und Trinkgeld noch dazu. Tumaini selbst baut eine Hühner-, Vieh- und Schweinezucht auf. Er hat inzwischen einen Wohlstandsbauch, den man als Kitambi bezeichnet, und einen PKW, damals beide Standessymbole. Von den Leuten wird er respektvoll mit „Mzee“ angesprochen.*

Wakati Tumaini alipokuwa akijijenga, siasa ya Tanzania ilikuwa ikienda moto moto. Baada ya Azimio la Arusha jina tu la Tanzania lilianza kuwa kitisho kwa wale wanaoabudu ubepari. Tumaini alikuwa amekwisha sikia habari nyingi juu ya Azimio hilo la Arusha lakini alifikiri liliwahusu hasa Wahindi, Wazungu na wanasiasa wenyewe.

Siku moja mkutano uliitishwa hapo mjini Shinyanga na mzungumzaji alikuwa mkuu fulani kutoka Dar es Salaam. Tumaini alikata shauri kuhudhuria mkutano huu – kama yeye alivyosema – kusikiliza ndoto za wanasiasa. (Uk. 167-168)

*Die Volksversammlung beginnt mit reichlicher Verspätung. Kinder weinen, Frauen beklagen sich, Männer schimpfen und alle leiden unter der glühenden Sonnenhitze. Nur die Verkäufer von Erdnüssen und Mais erfreuen sich eines guten Geschäftsgangs.*

Saa kumi na moja kamili msururu wa magari ya Waheshimiwa ulianza. Watu wakaanza kupiga makofi. Mheshimiwa kutoka Dar es Salaam alikuwa kwenye gari moja na Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa. Walipotoka tu garini makofi yaliongezeka mpaka walipopanda jukwani na Waheshimiwa wadogo kuchukua nafasi zao kando ya jukwaa hilo.

„Uhuru wananchi!“ Mkuu wa Wilaya aliwasalimu watu.

„Kazi ya TANU!“ walijibu.

„Mnajibu kama watu wenye njaa! Aliyetuletea njaa amekwishakwenda!

„Uhuru wananchi!“

„Kazi ya TANUUUU!“ walijibu kwa sauti ya juu sana.

„Mnapojibu hivyo mnanifurahisha sana; maana mnanihakikishia kwamba hamna njaa!“

Watu walicheka. Aliendelea.

„Na Watanzania hatuwezi kujenga taifa la wenye njaa.“ Alikohoa kidogo, halafu akaendelea,

„Mimi leo sitaki kuwambia maneno mengi, maana kama nikisema maneno mengi mkifika nyumbani mkiulizwa mmeambiwa nini, mtajibu, 'Aaa! Maneno mengi tu!' Mimi nitasema maneno machache ili mpate kufaidika na ujumbe atakaotwambia Mheshimiwa mgeni wetu. Lakini kabla ya Mheshimiwa kusema, Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa angependa kutoa salamu kwenu. Karibu Mheshimiwa!“

Makofi machache yalisikika pande zote Mkuu wa Mkoa aliposimama.

„Uhuru wananchi!“ Mkuu wa Mkoa alisema.

„Kazi ya TANUUUU!“

„Uhuru na Ujamaa!“

„Kazi ya TANUUUU!“

„Smith!“

„Ziiiiiii!“

„Kaburu!“

„Ziiiiiii!“

„Mreno“

„Ziiiiiii!“

„Bepari!“

„Ziiiiiii!“

„TANU!“

